THE NATIONAL ASSEMBLY
PAPERS LAID
DATE: 09 APR 2025 DAY. Wednesday
TABLED BY: Hon. Irene Mayaka MP Mwenyekiti
CLERK-AT THE-TABLE: A. Shibuko

Approved SNA 9/4/25

**JAMHURI YA KENYA**

**BUNGE LA KUMI NA TATU – KIPINDI CHA NNE**

**BUNGE LA TAIFA**

**KAMATI YA UTANGAMANO WA KIKANDA**

---

# RIPOTI YA KAMATI YA KIKANDA KUHUSU ZIARA YA UKAGUZI WA ASASI ZISIZOJITEGEMEA KIKAMILIFU ZA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI NA UKANDA WA KATI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**APRILI, 2025**

***Kurugenzi la Kamati za Ukaguzi, Kuidhinisha Matumizi na Kamati Nyingine za Kijumla***
*Majengo ya Bunge la Taifa*
**NAIROBI**

Contents

UFUPISHO ... 4

1.0 DIBAJI ... 7

1.1. Kuundwa na Wajibu wa Kamati ... 7

1.2. Uanachama wa Kamati ... 7

1.3. Ukatibu wa Kamati ... 9

2.0 ZIARA YA UKAGUZI WA ASASI ZISIZOJITEGEMEA KIKAMILIFU ZA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI NA UKANDA WA KATI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ... 10

2.1 Historia ... 10

2.2 Ujumbe ... 10

2.3 Malengo ya ziara ya ukaguzi ... 10

3.0 KAULI YA TUME ... 10

3.1 Dhima Kuu ya Tume ya Kiswahili ... 11

3.2 Muundo wa Tume ... 11

3.3 Mafanikio makuu ya Tume ... 12

3.4 Uundaji wa Mpango Mkakati wa Pili wa Tume ... 14

3.5 Changamoto Kuu ... 14

3.6 Mapendekezo kuhusu Mambo Muhimu ... 15

3.7 Mapendekezo zaidi ... 15

4.0 MIKUTANO NA ASASI ... 15

4.1 Kukutana na Wakenya wanaoishi na kufanya kazi Zanzibar ... 15

4.2 Mkutano na Balozi wa Kenya nchini Tanzania ... 16

4.2.1 Jiopolitiki ... 16

4.2.2 Muundo wa Kijamii na Kitamaduni ... 17

4.2.3 Usalama ... 17

4.2.4 Uhusiano wa Kenya na Tanzania ... 18

4.2.5 Miradi na Mipango muhimu ya pamoja ... 19

4.3 Masuala ya Kigeni na Kibalozi ... 19

4.4 Fursa kwa Kenya ... 20

4.4.1 Mradi wa gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa ... 20

4.4.2 Kukuza Biashara na Uwekezaji wa Pamoja ... 21

4.4.3 Kudumisha Uwepo wa Kidiplomasia wa Kenya wa Masoko Mapya na Ibuka ... 21

4.4.4 Utekelezaji wa Itifaki ya Jumuiya kuhusu Habari, Mawasiliano na Teknolojia ... 22

4.5 Masuala ya Utawala katika Balozi ... 22

4.5.1 Raslimali kazi ... 22

4.5.2 Fedha na makadirio ... 22

4.5.3 Usimamizi wa utendakazi ... 22

4.5.4 Mali za serikali ... 22

4.5.5 Magari ... 23

5.0 YALIYOGUNDULIWA ... 24

6.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO ... 25

VIAMBATISHO ... 26

**UFUPISHO**

| | |
|---|---|
| **AfCFTA** | African Continental Free Trade Area |
| **CMP** | Common Market Protocol |
| **EAC** | East African Community |
| **EACKC** | East Africa Kiswahili Commission |
| **GoK** | Government of Kenya |
| **RECs** | Regional Economic Communities |

## UTANGULIZI WA MWENYEKITI

Katika kuendeleza wajibu wa uangalizi wa Kamati ya Utangamano wa Kikanda na kulingana na kiu cha kuimarisha utangamano wa kikanda kupitia wawakilishi wa wananchi, katika kikao chake cha tarahe 3 Agosti 2023, Kamati iliamua kufanya ziara ya ukaguzi na kujifahamisha kwa asasi zisizojitegemea kikamilifu zifuatazo za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kutangamana na kamati zinazojihusisha na utangamano wa kikanda katika mabunge ya nchi wanachama:

1) Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, Zanzibar, Tanzania; na,
2) Bandari ya Dar es Salaam ambayo ni mwanzo wa Ukanda wa Kati.

Lengo kuu la ziara ni kuwafahamisha Wabunge kwa kazi ya asasi za Jumuiya na kutathmini kiwango cha utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali kwa madhumuni ya kutathmini na kubaini hatua zinazolenga kukuza utangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ziara hii iliwapatia Wabunge fursa ya kutangamana na kubadilishana tajriba na wenzao katika nchi wanachama.

Ujumbe wa Kamati ya Utangamano wa Kikanda ulifanya ziara ya ukaguzi wa Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki kati ya tarehe 24 na 29 Machi 2024. Lengo kuu la ziara lilikuwa ni kujifahamisha na jukumu la Tume la kuratibu na kukuza ustawi na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano na lugha rasmi ya Jumuiya. Hii ni kulingana na wajibu wa Kamati wa kuimarisha uhusishwaji wa Bunge katika kukoleza mchakato wa utangamano wa Jumuiya na bara la Afrika kwa jumla.

Ziara hii pia ilinuia kujua hatua zilizopigwa na Tume katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya na changamoto zake kwa lengo la kulifahamisha Bunge.

Tume hii iliundwa kutokana na dhima ya Kiswahili katika kuimarisha utangamano wa kikanda. Ibara ya 137 ya Mkataba wa Jumuiya inaelekeza kukuza ustawi na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano ya Jumuiya. Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume hii iliwekwa sahihi mnamo Aprili 2007. Tume iliundwa mnamo 2007 katika Kongamano la Tano la dharura na kuanza shughuli zake Julai 2015 mjini Arusha. EAKC ilihamia Zanzibar Machi 2016 kufuatia kutiwa sahihi kwa makubaliano na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka wa 2015.

Katika ziara hiyo, Kamati ilikuwa na mikutano ya mashauriano na ukatibu wa Tume hiyo ili kubadilishana mawazo na kujua changamoto wanazopata katika ustawi na utekelezaji wa sera za Kiswahili za kikanda. Pia Kamati ilikuwa na mikutano ya mashauriano na Wakenya wanaofanya kazi na kuishi Zanzibar. Ujumbe uligundua kuwa changamoto moja kuu Wakenya wanapata ni kulipa viza za kibiashara kila baada ya miezi mitatu. Hii ni licha ya kuwepo kwa mapatano yanayoruhusu uhuru wa kusambaza bidhaa na huduma. Suala hili linafaa kuangaziwa kidplomasia. Tofauti zilizoko katika ada za huduma za uchukuzi bandarini Tanzania zinafaa kushughulikiwa. Kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar,

Wakenya wanatakiwa kulipa Dola 35 za Marekani katika daraja la kawaida ilhali Watanzania wanalipa Tshs30,000 (Dola 10) peke yake. Suala hili linafaa kuangaziwa na Kamati ya Kiufundi ya Uchukuzi.

Kamati inapendekeza Kenya na Tanzania ziendelee kuboresha uhusiano mwema kwa kuimarisha mipango ya mara kwa mara ya ushirikiano. Kuimarishwa mahusiano haya kutaleta mazingira yanayofaa kustawisha utangamano na ushirikiano wa kikanda. Hivyo basi kuna haja ya mashaurino ya kidiplomasia na Serikali ya Tanzania yanayolenga kuzifanya sheria zake kuwezesha Wakenya kuwekeza.

Aidha, ujumbe ulikuwa na fursa ya kuzuru Ubalozi wa Kenya jijini Dar es Salaam na kuwa na mazungumzo ya kufana na balozi ambaye alihimiza wa Jumuiya dhabiti. Alisisitiza haja ya kufanya mikutano na kamati za Baraza la Mawaziri katika siku za usoni ili kutafuta mbinu za pamoja kusuluhisha vikwazo vya kiushuru vya kibiashara kabla ya Juni 2024. Mazungumzo yalisisitiza umuhimu wa kukuza ushirikiano wa kibiashara, ustawi wa miundomsingi, wa kijamii na wa kiuchumi katika kanda.

Ripoti hii ina mawasilisho, yaliyogunduliwa na mapendekezo kutoka kwenye ziara ya ujumbe wa Kamati ya Utangamano wa Kikanda iliyofanywa Zanzibar na Dar es Salaam, Tanzania kutoka Machi 24 hadi Machi 29, 2024. Kamati inashukuru uongozi wa Tume ya EAKC; Katibu Mtendaji, Dkt. Caroline Asiimwe, na Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Bw. Isaac Njenga kwa msaada wao adhimu wakati wa ziara hiyo.
Shukrani za dhati ziwaendee Spika na Katibu wa Bunge la Taifa kwa msaada wao adhimu kwa Kamati ilipokuwa ikitekeleza wajibu wake.

Kwa niaba ya Kamati ya Utangamano wa Kikanda na kwa mujibu wa Kanuni 212, ni furaha na wajibu wangu kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kikanda Kuhusu Ziara ya Ukaguzi wa Asasi Zisizojitegemea Kikamilifu za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ukanda wa Kati katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. DAVID OCHIENG, CBS, MBUNGE - KIONGOZI WA UJUMBE**

## 1.0 DIBAJI

### 1.1. Kuundwa na Wajibu wa Kamati

1. Kamati ya Utangamano wa Kikanda ni kamati ya Bunge la Taifa iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 212 ya Bunge la Taifa inayobainisha wajibu wa Kamati hii. Kamati iliundwa mnamo Oktoba 2023 baada ya Bunge la Taifa kuidhinisha Hoja kuhusu uanachama wa kamati zake. Kamati inajumuisha wanachama 21 ambao watahudumu kwa Muhula wa Bunge la 13.
2. Aidha, Kamati ya Utangamano wa Kikanda inawajibika
   (a) Kuimarisha jukumu na uhusika wa Bunge la Taifa la Taifa katika kuzidisha na kustawisha mchakato wa utangamano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika nzima;
   (b) Kutathmini kumbukumbu za mijadala yote inayohusika na maamuzi ya mikutano yote ya Bunge la Afrika Mashariki;
   (c) Kutathmini Miswada iliyowasilishwa kwenye Bunge la Afrika Mashariki na Sheria za Jumuiya ya Afrika Mashariki;
   (d) Kutathmini kumbukumbu za mijadala yote inayohusika na maamuzi ya mikutano yote ya Bunge la Afrika, Baraza la Pamoja la Mabunge ya Afrika, Visiwa vya Karibi na Pasifiki-Umoja wa Ulaya na mashirika mengine ya utangamano wa kikanda; na
   (e) Kuchunguza na kutathimini suala lingine lolote linalohusiana na utangamano wa kikanda linalohitajika kushughulikiwa na Bunge la Taifa.

### 1.2. Uanachama wa Kamati

3. Kamati inajumuisha wanachama wafuatao

Mhe. Wanjiku Muhia, MP – Mwenyekiti
Eneobunge la Kipipiri
**United Democratic Alliance**

Mhe. Farah Salah Yakub, MP – Naibu Mwenyekiti
Eneobunge la FAFI
**United Democratic Alliance**

Mhe. David Ochieng Ouma, Mbunge
Eneobunge la Ugenya
**Movement for Democracy and Growth**

Mhe. Geoffrey Makokha Odanga, Mbunge
Eneobunge la Matayos
**Orange Democratic Party**

Mhe. Naomi Jillo Waqo, Mbunge
Kaunti ya Marsabit (CWR)
**United Democratic Alliance**

Mhe. Joseph Gachoki Gitari, Mbunge
Eneobunge la Kirinyaga ya Kati
**United Democratic Party**

Mhe. Christopher Aseka Wangaya, Mbunge
Eneobunge la Khwisero
**Orange Democratic Party**

Mhe. Danson Mwashako Mwakuwona, Mbunge
Eneobunge la Wundanyi
**Wiper Democratic Movement**

Mhe. Andrew Adipo Okuome, Mbunge
Eneobunge la Karachuonyo
**Orange Democratic Party**

Mhe. Rael Chepkemoi Kasiwai, Mbunge
Kaunti ya West Pokot (CWR)
**Kenya Union Party**

Mhe. Peter Ochieng Orero, Mbunge
Eneobunge la Kibra
**Orange Democratic Alliance**

Mhe. Elizabeth Karambu Kailemia, Mbunge
Kaunti ya Meru (CWR)
**United Democratic Alliance**

Mhe. Julius Kipletting Rutto, Mbunge
Eneobunge la Kesses
**United Democratic Party**

Mhe. Beatrice Chepng'eno Kemei, Mbunge
Kaunti ya Kericho (CWR)
**United Democratic Alliance**

Mhe. Fatuma Hamisi Masito, Mbunge
Kaunti ya Kwale (CWR)
**Orange Democratic Party**

Mhe. Peter Kalerwa Salasya, Mbunge
Eneobunge la Mumias Mashariki
**Democratic Alliance Party**

Mhe. Irene Njoki Mrembo, Mbunge
Eneobunge la Bahati
**Jubilee Party**

Mhe. Richard Kipkemoi Yegon, Mbunge
Eneobunge la Bomet Mashariki
**United Democratic Alliance**

Mhe. Didmus Wekesa Barasa Mutua, Mbunge
Eneobunge la Kimilili
**United Democratic Alliance**

Mhe. Zaheer Jhanda, Mbunge
Eneobunge la Nyaribari Chache
**United Democratic Party**

Mhe. Japheth Nyakundi Mokaya, Mbunge
Eneobunge la Kitutu Chache Kaskazini
**United Democratic Party**

### 1.3. Ukatibu wa Kamati

4. Ukatibu unaohudumia Kamati hii ni kama ifuatavyo: –

| | | |
|---|---|---|
| Bw. Mohamed Jimale | - | Katibu Msaidizi I (Kiongozi) |
| Bi. Jane Gathoni Ouko | - | Katibu Msaidizi III |
| Bw. Bernard Toroitich | - | Katibu Msaidizi III |
| Bw. Dominic Kyallo | - | Wakili II |
| Bw. Damacrine Kwamboka | - | Afisa wa Utafiti III |
| Bw. Moses Kariuki | - | Mpambe wa Bunge |
| Bi. Mercy Mayende | - | Afisa wa Mahusiano na Vyombo vya Habari III |

## 2.1 ZIARA YA UKAGUZI WA ASASI ZISIZOJITEGEMEA KIKAMILIFU ZA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI NA UKANDA WA KATI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### 2.2 Historia

5. Kamati ya Utangamano wa Kikanda ni kamati ya Bunge la Taifa iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 212 ili, pamoja na mengine, kuimarisha jukumu na uhusika wa Bunge la Taifa katika kukoleza na kustawisha mchakato wa utangamano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Afrika nzima na kuchunguza na kutathmini suala lingine lolote linalohusiana na utangamano wa kikanda linalohitajika kushughulikiwa na Bunge la Taifa.

6. Katika mkutano wake uliofanyika Alhamisi 8 Machi 2024, Kamati iliamua kufanya ziara ya ukaguzi katika EAKC, Bandari ya Zanzibar, Bandari ya Dar es Salaam, na kufanya ziara ya heshima kwa afisi ya Balozi wa Kenya nchini Tanzania.

7. Ujumbe uliojumuisha Wabunge watano ulizuru EAKC na Ubalozi wa Kenya jijini Dar es Salaam ilivyoratibiwa kuanzia tarehe 24 hadi 29 Machi 2024. Kulingana na ratiba ya ziara yenyewe, ujumbe haukuweza kutembelea Bandari ya Zanzibar na Bandari ya Dar es Salaam kwa sababu zisizoepukika.

### 2.3 Ujumbe

8. Kamati iliamua kufanya ziara ya ukaguzi na kujifahamisha kuhusu hali/kiwango cha utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali kwa madhumuni ya kutathmini na kubaini hatua zinazolenga kukuza utangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

   a) Mhe. David Ochieng, Mbunge - **Kiongozi wa Ujumbe**
   b) Mhe. Christopher Aseka, Mbunge
   c) Mhe. Joseph Gitari, Mbunge
   d) Mhe. Beatrice Kemei, Mbunge
   e) Bw. Dominic Mwendwa - Wakili II/Katibu wa Ujumbe

### 2.4 Malengo ya ziara ya ukaguzi

9. Lengo la ziara ya ukaguzi lilikuwa kubainisha hatua zilizopigwa na asasi zisizojitegemea kikamilifu za jumuiya pamoja na eakc katika kuratibu na kueneza ustawishaji na matumizi ya kiswahili katika kanda na kwingineko. Hii ni muhimu kwa sababu eakc ni mojawapo ya asasi zisizojitegemea kikamilifu za jumuiya iliyokabidhiwa wajibu wa kuhakikisha ustawi wa kiswahili kama lugha ya mawasiliano kwa ajili ya mwingiliano wa kikanda na kimataifa ili kujistawi kisiasa, kitamaduni, kielimu, kisayansi, na kiufundi.

## 3.0 KAULI YA TUME

10. Ujumbe ulizuru EAKC tarehe 25 Machi 2024. Katibu Mtendaji alifahamisha Ujumbe kuwa Eakc ni asasi maalum ya Jumuiya ambayo wajibu wake ni kuratibu na kukuza ustawi na matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya mawasiliano.

11. Katibu Mtendaji alitaja kuwa Tume ya Kiswahili iliundwa kwa sababu ya umuhimu wa Kiswahili katika kuendeleza utangamano wa kikanda kwa mujibu wa Ibara 137 ya Mkataba

wa Jumuiya inayoelekeza ustawi na matumizi ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano ya Jumuiya.

12. Itifaki ya Kuanzishwa kwa Tume hii ilitiwa sahihi mnamo Aprili 2007. Tume iliundwa mnamo 2007 katika Kongamano la Tano la Dharura na kuanza shughuli zake Julai 2015 mjini Arusha. EAKC ilihamia Zanzibar Machi 2016 kufuatia kutiwa sahihi kwa Makubaliano na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka wa 2015.

### 3.1 Dhima Kuu ya Tume ya Kiswahili

13. Katibu Mtendaji alieleza Ujumbe kwamba dhima kuu ya EAKC ni kushauri Jumuiya kuhusu masuala yote yanayohusu Kiswahili.

14. Kulingana na Katibu Mtendaji, dhima nyingine za EAKC ni—

a) Kuratibu na kusimamia kazi ya Mabaraza ya Taifa ya Kiswahili na asasi nyinginezo;

b) Imarisha ushirikiano katika tafiti za kikanda.

c) Kusaidia nchi wanachama kuanzisha vituo vya masomo ya juu na vya utafiti wa Kiswahili.

d) Kuanzisha ushirikiano na washirika wa kimaendeleo na mashirika yaliyopo yenye malengo sawa.

e) Kuwezesha ustawi wa sera za Kiswahili za kikanda za ubadilishanaji wa wafanyakazi na wanafunzi katika taasisi za Kiswahili na kufuatilia ufanisi wa sera hizo.

f) Kutambua mahitaji ya mafunzo ya Kiswahili ikiwemo uhakiki wa mtalaa, mbinu za mafunzo, kutengeza vifaa vya ufundishaji na utafiti;

g) Kutetea matumizi ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano ndani na nje ya Jumuiya;

h) Kuhimiza matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi; na,

i) Kutekeleza majukumu yoyote mengine kuendeleza malengo ya Tume jinsi Baraza linavyoweza kuelekeza.

### 3.2 Muundo wa Tume

15. Tume ya EAKC inajumuisha wawakilishi wafuatao:

a) Wawakilishi wawili wa Baraza la Taifa la Kiswahili la kila nchi mwanachama;

b) Wawakilishi wawili wa Miungano Ya Kiswahili ya kila nchi mwanachama;

c) Mwakilishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kiswahili ya kila nchi mwanachama;

d) Mwakilishi wa idara ya Kiswahili kutoka vyuo vya umma na vya kibinafsi katika kila nchi mwanachama;

e) Mwakilishi wa vyombo vya habari vya Kiswahili kutoka kila nchi mwanachama;

f) Mwakilishi wa Baraza la Wanahabari kutoka kila nchi mwanachama;

g) Mwakilishi wa Muungano wa Waandishi wa Kiswahili kutoka kila nchi mwanachama;

h) Mwakilishi wa Wizara inayohusika na Kiswahili kutoka kila nchi mwanachama;

i) Mwakilishi wa Wizara inayohusika na Utamaduni kutoka kila nchi mwanachama; na,

j) Mwakilishi wa Wizara inayohusika na Elimu kutoka kila nchi mwanachama.

### 3.3 Mafanikio makuu ya Tume

16. Tangu kuanzishwa kwake, Tume ya EAKC imefanikiwa kufanya yafuatayo:

a. **Kongamano la Kiswahili la Kimataifa la EAKC** – EAKC huandaa Kongamano la Kiswahili la Kimataifa mara mbili kwa mwaka. Linaleta pamoja watafiti, wataalamu na washikadau ili kubadilishana maarifa na ujuzi kuhusu matukio ibuka katika ulingo wa Kiswahili. Kongamano la Kiswahili la Kimataifa la kwanza lilifanyika Zanzibar mwaka wa 2017 ilhali la pili liliathirika na janga la Covid 19. Kongomano hilo limeratibiwa kufanyika Nairobi, Kenya tarehe 7 Julai 2024.

b. **Tathmini ya Ustawi na Matumizi ya Kiswahili ndani ya Jumuiya** – EAKC ilifanya tathmini katika nchi wanachama wa Jumuiya ili kujua uwezo na changamoto ambazo zinakumba nchi wanachama katika kukuza na kustawisha Kiswahili. Ripoti hiyo iliandikwa na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri la 38. Ripoti hiyo imesaidia Eakc kuchukua hatua; na,

c. **Tume ilifanya utafiti/uchanganuzi kubaini mahitaji ya mafunzo katika nchi wanachama wa Jumuiya** ili kutambua changamoto zinazokabili ustawi na ukuzaji wa Kiswahili katika Jumuiya. Uchambuzi ulifanyika kutambua mahitaji muhimu ya mafunzo yanayofaa kupewa kipaumbele na Eakc. Ikishauriana na nchi wanachama, Tume ilibaini mahitaji muhimu ya mafunzo ya Kiswahili ya kila nchi mwanachama.

**i. Jamhuri ya Burundi**

a) Mafunzo ya Kiswahili kwa walimu wa shule za msingi na upili;

b) Mafunzo ya Kiswahili kwa wafanyakazi wa umma; na,

c) Mafunzo ya Kiswahili kwa wanahabari.

**ii. Jamhuri ya Kenya**

a) Mafunzo ya Kiswahili kwa Bunge;

b) Mafunzo ya Kiswahili kwa wanahabari;

c) Mafunzo ya Kiswahili kwa Mahakama.

**iii. Jamhuri ya Rwanda**

a) Mafunzo ya Kiswahili kwa minajili ya biashara (SMEs);

b) Mafunzo ya Kiswahili kwa wanahabari;

c) Mafunzo ya Kiswahili katika sekta ya elimu (vyuo vya mafunzo ya walimu).

**iv. Jamhuri ya Sudan Kusini**

a) Kufunza walimu wa Kiswahili katika shule za upili;

b) Kufunza Kiswahili kama lugha ya kimataifa; na,

c) Mafunzo ya Kiswahili kwa wanahabari;

**v. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

a) Kufunza wataalamu kufunza Kiswahili kama lugha geni;

b) Mafunzo ya Kiswahili kwa wanahabari;

c) Mafunzo ya Kiswahili kwa tasnia ya ubunifu.

**vi. Jamhuri ya Uganda**

a) Mafunzo ya Kiswahili kwa Bunge;

b) Mafunzo ya Kiswahili kwa wanahabari;

c) Mafunzo ya Kiswahili kwa sekta ya elimu.

d. **Kuunda mipango na miongozo ya mafunzo ya Kiswahili** – Tume iliunda mipango na miongozo ya kufunza Kiswahili ili kukidhi mahitaji ya Kiswahili ya nchi wanachama. Miongozo na mipango inajumuisha:

i. Mipango ya Mafunzo ya Kiswahili kwa wataalamu kufunza Kiswahili kwa watumizi wa lugha nyingine katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Mipango ya Mafunzo ya Kiswahili kwa Bunge la Uganda;

iii. Mipango ya Mafunzo ya Kiswahili kwa Bunge la Kenya;

iv. Mipango ya Mafunzo ya Kiswahili kwa walimu wa Kiswahili katika shule za upili nchini Sudan Kusini;

v. Mafunzo ya Kiswahili kwa Walimu wa Shule za Msingi na upili nchini Burundi; na,

vi. Mafunzo ya kiswahili kwa minajili ya biashara (smes) nchini Rwanda.

e. **Kufunza wakufunzi watakaotekeleza mipango ya mafunzo ya kiswahili** – Tume ilifunza wakufunzi 60 watakaotekeleza mipango ya mafunzo ya kiswahili katika nchi wanachama. Wakufunzi 10 kwa kila nchi mwanachama walihudhuria mafunzo yaliyowapa ustadi na weledi wa kufunza wengine kutekeleza mipango ya mafunzo kwa ufanisi. Mafunzo kwa wakufunzi yalifanyika baada ya nchi wanachama kumaliza na kuidhinisha mipango na miongozo ya mafunzo ya kiswahili.

f. **Kuunda mipango na sera ya ubadilishanaji** – Tume iliunda mipango na sera ya ubadilishanaji wa wafanyakazi, wanafunzi, maafisa wa serikali, wanahabari, wanaharakati na wafanyabiashara. Tume ilidhamini washikadau 26 katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mipango hiyo. Sera hiyo imechangia kuimarisha Kiswahili katika nchi wanachama zilizokuwa na changamoto.

g. **Ushirikiano** – Tume inalenga ushirikiano wa kimkakati utakaochangia utekelezaji wa shughuli, kuhamasisha/kuchanga/kukusanya raslimali na uonekanaji/uwepo. Kupitia ACALAN, Tume inashirikiana na Umoja wa Afrika kutekeleza Mfumo wa Dar es Salaam wa Utekelezaji wa Kutambua na Kukuza Kiswahili Barani Afrika. Tume imeanzisha ushirikiano na MSTCDC, UNESCO, Howard University-USA, na Wakfu wa SAFAL Group na mashirika mengine. Inafanya kazi na mashirika mengine ya kikanda yanayothamini Kiswahili.

h. **Vituo vya masomo ya juu na utafiti wa Kiswahili** – EAKC imepewa wajibu wa kusimamia kuanzishwa kwa vituo vya juu na utafiti wa Kiswahili katika nchi wanachama. Pia imeunda kanuni na miongozo ya uanzishwaji wa vituo hivi ambavyo vilizingatiwa na SCESTCS. Aidha, Tume inatafuta rasilimali za kuanzisha vituo hivi.

i. **Utafiti na Uchapishaji** – Tume ina wajibu wa kuratibu utafiti wa Kiswahili na imechangia machapisho kadhaa kuhusu masuala ibuka ya Kiswahili. Tume inafadhili utafiti wa Kiswahili kwa kupeana misaada kwa wanafunzi wa shahada za juu kutoka nchi wanachama. Lengo kuu ni kuimarisha utafiti katika Kiswahili. Hata hivyo, pana haja ya kufadhili zaidi watafiti wachanga. Ilivyo kwa sasa, Tume inawafadhili wanafunzi wa shahada za juu kutoka nchi wanachama kufanya tafiti zao.

j. **Kutafsiri stakabadhi za Jumuiya kwa Kiswahili** – Wajibu mojawapo wa Tume ni kutafsiri stakabadhi muhimu za Jumuiya kwa Kiswahili ili kuwawezesha wananchi wengi kuelewa stakabadhi hizo. Tume ilitafsri Mkataba wa EAC kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, na nakala hiyo ikazingatiwa na Baraza la 15 la Elimu, Sayansi na Teknolojia, Utamaduni na Michezo na kutumwa kwa nchi wanachama zitoe maoni. Tayari maoni yamepokewa na kinachosubiriwa ni hela ili kukamilisha shughuli hiyo.

k. **Utekelezaji wa Kiswahili kama Lugha Rasmi ya Jumuiya** – Kongamano la 21 la Marais wa nchi wanachama lilitangaza Kiswahili kama lugha rasmi ya Jumuiya na kuamuru kuwe na mpango wa kutekeleza amri hiyo. Tume iliunda mpango huo ambao uliidhinishwa na mkutano wa 17 wa SCESTCS na Baraza la 42. Kongamano la Marais liliamuru mpango huo utekelezwe haraka. Tume imeanza kuutekeleza mpango huo.

l. **Kuadhimisha Siku ya Kiswahili Duniani** – Mnamo Novemba 2021, UNESCO iliteua kila tarehe 7 Julai kuwa Siku ya Kiswahili Duniani. Baraza la Jumuiya liliridhia na kuamrisha maadhimisho haya yafanywe kila mwaka kwa mzunguko katika nchi wanachama. Maadhimisho ya kwanza ya Jumuiya ya Siku ya Kiswahili yaliandaliwa Zanzibar Julai 2022; ya pili, Kampala, Uganda Julai 2023; na, ya tatu yanatarajiwa kufanywa Kenya Julai 2024.

### 3.4 Uundaji wa Mpango Mkakati wa Pili wa Tume

17. Katibu Mtendaji alisema kwamba muda wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kwanza (2017 – 2022) umeisha. Hata hivyo, Tume inaunda Mpango Mkakati wake wa Pili ambao utaongoza utekelezaji wa shughuli za Tume kwa miaka mitano ijayo.

18. Aidha, iliripotiwa kwamba mashauriano na washika dau kutoka nchi wanachama yamepangwa kufanyika Aprili 2024.

### 3.5 Changamoto Kuu

19. Katika wasilisho lake, Katibu Mtendaji alitaja changamoto kadhaa ambazo Tume inakumbana nazo katika shughuli zake kama ilivyoorodheshwa kwenye Mkataba.
20. Changamoto kuu zilizotajwa ni zifuatazo—
    a) Uhaba wa wafanyakazi unaoathiri utendakazi wake;
    b) uhaba wa fedha za kutekeleza shughuli zake;
    c) uwezo duni wa kukusanya raslimali;
    d) kutokuwepo kwa bodi ya utawala kunachelewesha maamuzi kufanywa;
    e) nchi wanachama kuchelewa kutoa michango yao;
    f) kuchelewa kukamilisha Mswada wa EAKC;
    g) kutokuwepo kwa Mabaraza ya Taifa ya Kiswahili katika baadhi ya nchi wanachama; na,
    h) kutokuwepo kwa Sera za Taifa za Kiswahili.

### 3.6 Mapendekezo kuhusu Mambo Muhimu

21. Majadiliano baina ya wasimamizi wa Tume na Wajumbe yalitambua yafuatayo kuwa muhimu ili Tume iboreshe wajibu wake. Nayo ni—
    a) Kuundwa kwa bodi ya utawala ili kuimarisha utawala na kufanya maamuzi;
    b) kuharakisha mchakato wa kurekebisha Mkataba ili Kiswahili kiwe moja ya lugha rasmi za Jumuiya;
    c) kuharakisha mchakato wa kurekebisha itifaki ya EAKC ili kukidhi mahitaji ibuka ya Tume;
    d) kuongeza mgao kwa Tume ili kutekeleza majukumu muhimu;
    e) kuharakisha utunzi na kupitishwa kwa Mswada wa EAKC (CTC kuharakisha utunzi wa Mswada huo);
    f) kumaliza hatua za kupokeza EAKC kwa Jumuiya. Tume ianze utekelezaji wa Kiswahili kama lugha rasmi ya Jumuiya;
    g) Tume iwezeshe uhamasisho na ueneaji wa umaarufu wake kwa washikadau muhimu;
    h) kuhakikisha wafanyakazi wanateuliwa katika nafasi muhimu.

### 3.7 Mapendekezo zaidi

22. Pamoja na ya awali, wajumbe wanapendekeza kwamba—
    a) Tume iweke mikakati ya kukuza Kiswahili katika Jumuiya kama lugha ya mawasiliano na lugha ya ustawi;
    b) Kenya inafunza Kiswahili kama lugha ya lazima katika shule zake za msingi na upili ndiposa karibu kila Mkenya anaweza kuzungumza Kiswahili. Shule za nchi wanachama zafaa kuiga hili sawasawa na Ibara ya 7 ya Mkataba inayotambua Kiingereza na Kiswahili kama lugha rasmi;
    c) Tume ihamasishe umma wa nchi wanachama kuhusu hatua zake zinazokusudia kuinua hadhi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya mawasiliano. Mipango hiyo inafaa kuwekwa wazi na nchi wanachama kupata taarifa hiyo kwa urahisi;
    d) Tume ilenge kusanifisha Kiswahili na kutafsiri stakabadhi zaidi za Jumuiya, kando na Wimbo wa Jumuiya. Maamuzi ya Baraza yawe katika Kiswahili na Kiingereza, na;
    e) Tume ihimize stakabadhi za EALA na hukumu za EACJ ziwe kwa Kiswahili na Kiingereza.

## 4.0 MIKUTANO NA ASASI

### 4.1 Kukutana na Wakenya wanaoishi na kufanya kazi Zanzibar

23. Maafisa wa Ubalozi waliandaa mkutano na Wakenya wanaoishi na kufanya kazi Zanzibar ambao ulifanyika katika viwanja vya EAKC.
24. Wakenya wanaofanya kazi Zanzibar wanakabiliana na changamoto nyingi ambazo waliomba Wajumbe waingilie kati.
25. Yafuatayo ni baadhi ya maswala waliyoibua:
    a) Tofauti na Kenya ambayo haitozi wananchi wa Jumuiya vibali vya kazi, Tanzania hutoza Wakenya.

b) Viza za kufanya biashara ni ghali mno, dola 100 za Marekani, na hutolewa mipakani tu kila baada ya miezi mitatu hivyo kulazimu Wakenya kusafiri hadi mipakani kila baada ya miezi mitatu ili kupata viza nyingine mpya. Aidha viza hizo huchukuliwa zimeisha muda wake punde mtu anapoondoka Tanzania kabla miezi hiyo mitatu kuisha hata kama anaenda kushughulikia dharura yoyote nchini Kenya.

c) Mkenya huhitajika kuwa na mtaji wa kazi ama mtaji wa hisa wa Tsh100,000,000 (Ksh5,800,000) ili kuanzisha kampuni Zanzibar. Hili linawanyima Wakenya fursa ya kusajili biashara za wastani na kuwalazimu kufanya biashara kwa kutumia kampuni zilizosajiliwa na wenyeji. Pia inawanyima kupata mikopo ya kupanua biashara zao kutoka Kenya na Tanzania.

d) Kupata kadi ya SIM ya viza ya biashara ni changamoto kubwa. Kadi hiyo huisha muda wake baada ya miezi mitatu hivyo kumlazimu mtu kurudia mchakato uleule anapotaka kusajili viza yake ya biashara tena; na,

e) Kulikuwa na kisa cha wakili mmoja Mkenya aliyesomea Chuo cha Sheria cha Zanzibar ambaye alinyimwa kibali cha kujiunga rasmi na taaluma/kazi kwa kukosa kitambulisho cha Tanzania bara.

26. Wajumbe, kupitia kwa Mwenyekiti, walijitolea kufanya kikao na Waziri wa Leba na Waziri anayeshugulika na mambo ya Jumuiya ili kuwafahamisha changamoto hizi na kupata suluhu.

27. Ujumbe pia uliahidi kutatua swala hilo na Balozi. Wajumbe walisema kibali cha biashara kinafaa kiwe cha muda wa mwaka mmoja.

### 4.2 Mkutano na Balozi wa Kenya nchini Tanzania

28. Ujumbe ulimtembelea Balozi wa Kenya nchini Tanzania tarehe 28 Machi 2024. Balozi aliwakaribisha Wajumbe na kuonyesha furaha yake kwa ziara hiyo iliyonuia kutathmini mchango wa Ubalozi katika kuendeleza utangamano na utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya.

29. Katika mazungumzo hayo, Balozi aliwasilisha yafuatayo:

#### 4.2.1 Jiopolitiki

30. Balozi aliwasilisha kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Inapakana na Uganda kaskazini; Kenya kaskazini mashariki; Visiwa vya Ngazija na Bahari Hindi upande wa mashariki; Msumbiji na Malawi upande wa Kusini; Zambia upande wa kusini-magharibi; na Rwanda na Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo upande wa magharibi. Ukubwa wa ardhi ni takriban kilomita mraba 947,303 na mwambao wa takriban kilomita 1,500.

31. Aidha, alisema kwamba Tanzania ni muungano kati ya Tanganyika (bara) na Zanzibar (kisiwa). Muungano huu ulindwa mnamo tarehe 26 Aprili 1964. Tanganyika ilipata uhuru mnamo 9 Desemba 1961 ilhali Zanzibar ilipata uhuru 10 Desemba 1963;

32. Kwa mujibu wa Balozi, nchi mwenyeji ina maeneo 26 na visiwa vitano. Maeneo hayo yamegawanywa kwa wilaya, tarafa na kata. Kila eneo linaongozwa na kamishna anayeteuliwa na rais. Nchi hiyo ina mfumo wa vyama vingi. Uchaguzi unafanywa kila baada ya miaka mitano na kulingana na katiba, na Rais wa Muungano huchaguliwa kupitia kwa kura na huhudumu kwa hadi mihula miwili.

33. Balozi pia aliwasilisha ifuatavyo:

a) Kura hupigwa katika kiwango cha serikali cha taifa na serikali za mitaa. Serikali za mitaa hupiga kura ya wenyekiti wa vijiji. Rais na Wabunge huchaguliwa katika uchaguzi mkuu. Uchaguzi mkuu wa mwisho ulifanyika Oktoba 2020 ambapo hayati Pombe Maghufuli alichaguliwa. Alishinda kwa asilimia 84 ya kura zote zilizopigwa na akawa rais wa awamu ya tano. Uchaguzi huo ulikuwa na wagombea kumi na wanne wa urais na uchaguzi mkuu ujao umepangwa kufanyika 2025 na uchaguzi wa serikali za mitaa umepangwa kufanyika Oktoba 2024.

b) Bunge ni moja na lina Wabunge 393 ambapo kati yao 264 wamechaguliwa kwa muhula wa miaka mitano. Nafasi maalum 113 zimetengewa wanawake. Wabunge kumi huteuliwa na rais ilhali nafasi tano hutengewa Bunge la Zanzibar na Mkuu wa Sheria. Bunge la Taifa hutunga sheria ambazo huongoza mahusiano baina ya Tanzania bara na muungano wote na nchi zingine. Bunge la Zanzibar nalo hutunga sheria ambazo hutumika Zanzibar pekee; na,

c) Rais humteua Waziri Mkuu ambaye anahuduma kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Nchi ina vyama 18 vilivyosajiliwa na Chama Cha Mapinduzi kimeongoza tangu uhuru. Chama cha uhuru, Tanganyika African Union (TANU), kilibadilika kuwa Chama Cha Mapinduzi baada ya kuungana na Afro-Shirazi Party (ASP) mwaka wa 1977.

### 4.2.2 Muundo wa Kijamii na Kitamaduni

34. Balozi alisema kuwa kuelewa muundo wa kijamii na kitamaduni wa nchi mwenyeji ni kanuni ya kimsingi katika mahusiano ya kimataifa kwani huwezesha balozi kuunda mikakati inayoafiki na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia.

35. Alisema kuwa falsafa ya kitaifa ya Ujamaa aliyoasisi Mwalimu Julius Nyerere ingali msingi wa jamii ya Tanzania ambapo kila rika na jamaa huwa na uzalendo mkubwa. Kulingana na sensa ya watu na nyumba ya 2022, idadi ya watu ni 61,741,120 ikijumuisha Waislamu, Wakristo na Watamaduni. Tanzania ina zaidi ya kabila 121 zinazoungana na kutangamana vyema.

36. Kiswahili na Kiingereza ndizo lugha rasmi za Tanzania bara ilhali Kiarabu kimeenea (kinazungumzwa sana) Zanzibar.

### 4.2.3 Usalama

37. Balozi alisema kuwa usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mzuri.

38. Tisho pekee kwa usalama wa Tanzania ni makundi ya wanamgambo kutoka Msumbiji Kaskazini Mkoa wa Cabo Delgado. Ili kuzuia uvamizi wa makundi hayo, Jamhuri ya Muungano imeweka vikosi vya usalama eneo la kusini la Ruvuma pande zote za mpaka. Wanamgambo hao hulenga Tanzania kwa sababu huchangia vikosi vya kudumisha amani katika mpango wa SAMM (Southern African Development Mission in Mozambique) unaotarajiwa kukamilika katikati ya Julai 2024 bila mafanikio makubwa. Huenda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikakumbwa na changamoto nyingine za kiusalama kutoka kwa makundi ya Kiislamu baada ya Julai

39. Pamoja na Malawi na Afrika Kusini, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia imechangia vikosi vya kudumisha amani mashariki mwa DRC. Operesheni hii inagonganisha vikosi vya SADC dhidi ya vikosi vya waasi hasa vile vya M23.

40. Majeshi ya Kenya na yale ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yamedumisha ushirikiano na uhusiano mwema wa kikazi kwa muda mrefu katika kubadilishana taarifa, mahusiano kupitia mfumo wa Jumuiya, mafunzo ya nchi mbili, na mipango ya kubadilishana wakufunzi na wanafunzi wa vyuo vya kitaifa vya kijeshi.

41. Sehemu nyingine za ushirikiano ni mafunzo ya kimataifa ya kudumisha amani, michezo ya kitamaduni ya Jumuiya, ziara, vita dhidi ya ugaidi, na kutumwa kwa washauri wa masuala ya ulinzi katika nchi zote mbili.

#### 4.2.4 Uhusiano wa Kenya na Tanzania

42. Balozi alisema Kenya na Tanzania zina uhusiano mwema wa kihistoria kutokana na kwamba zinapakana, zina jamii zenye utamaduni unaofanana, zinafanya biashara pamoja na zina malengo ya kufanana kwa Jumuiya. Uhusiano huu umeimarishwa zaidi na Ziara Rasmi za kiserikali kutoka pande zote mbili.

43. Alisisitiza kwamba Tanzania ni mshirika muhimu wa Kenya katika nyanja nyingi hasa biashara, usalama, elimu, kilimo, miundomsingi na kawi. Kenya na Tanzania zinashirikiana katika Mradi wa Ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki unaofadhiliwa na AfDB. Mradi huo unalenga kuunganisha Kenya na Tanzania, yaani barabara ya Malindi – Mombasa – Lunga Lunga/Horohoro na Tanga - Pangani - Bagamoyo (kilomita 454).

44. Aidha, Balozi alisema yafuatayo—

a) Chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kenya na Tanzania zina vituo vitatu vya mpakani vya huduma zote (OSBP) vilivyo Namanga, Lunga Lunga/Horo Horo na Taita Taveta/Holili na kile ambacho kitazinduliwa Isebania hivi karibuni;

b) Kikao cha kwanza cha Tume ya Pamoja ya Ushirikiano ya Kenya/Tanzania (JCC) kilifanywa Arusha, Tanzania mnamo September 2009. Tangu hapo, kumekuwa na vikao vingine vitatu.

c) Kikao cha majuzi cha JCC, ambacho ni cha nne, kilifanywa Agosti 2021 jijini Nairobi, Kenya. Tathmini ya Katikati ya Muhula wa JCC ulifanywa January 2023. Kikao cha tano cha JCC kilifanywa Agosti 2024;

d) Kenya na Tanzania zina Makubaliano ya Pamoja kuhusu Upitishaji Huru wa Bidhaa katika mipaka yao (yalitiwa sahihi tarehe 22 Mei 2020);

e) Tanzania ni mshirika muhimu na mkuu wa Kenya katika biashara na uwekezaji katika eneo hili na duniani. Kwa muda sasa, imekuwa nchi ya pili ambayo Kenya huuza bidhaa zake kwa wingi baada ya Uganda. Itifaki ya Forodha ya Jumuiya inaongoza nchi hizi mbili katika mahusiano yao kibiashara na kanuni zao za uwekezaji kwani itifaki hiyo ina mamlaka kuliko sheria za nchi binafsi.

f) Tanzania ni miongoni mwa nchi kumi za kwanza duniani ambazo Kenya huuza bidhaa zake. Bidhaa zinazouzwa Tanzania ziliongezeka kwa asilimia 17 mwaka wa 2022, hadi Dola 479.57 milioni za Marekani, kiwango ambacho ni asilimia 6.5 ya bidhaa zote zilizouzwa na Kenya kimataifa. Vivyo hivyo Kenya ni miongoni mwa nchi kumi za kwanza duniani ambako Tanzania huuza bidhaa zake. Bidhaa

zinazouzwa na Tanzania nchini Kenya zilipungua kwa asilimia 4, hadi Dola 381.66 milioni za Marekani, kiwango ambacho ni asilimia 5.6 ya bidhaa zote zilizouzwa na Tanzania kimataifa.

g) Bidhaa zinazouzwa na Kenya nchini Tanzania zinajumuisha: dawa; sabuni na bidhaa nyingine za usafi; mabamba ya chuma na chuma cha pua kisichochanganywa; mafuta; vifaa vya umeme; siagi; mafuta yanayoliwa ya wanyama na mimea; vitafunio vilivyo na sukari; mifuko; vizibo, vikofia na vifuniko; chumvi ya kupikia, magadi na chumvi safi;

h) Bidha zilizoagizwa kutoka Tanzania hadi Kenya zilikuwa na thamani ya Ksh25.8 bilioni mwaka wa 2020, punguzo dogo kutoka Ksh27.5 bilioni mwaka wa 2019. Bidhaa zilizoagizwa kutoka Tanzania hadi Kenya ni mahindi; bidhaa za karatasi; keki za makapi; kauri na vigae ghafi; magunia na mikoba; mbao za safu; bidhaa za kioganiki za usafi (isipokuwa sabuni) na kadhalika;

i) Kampuni zaidi ya 529 za Kenya zimewekeza takriban Dola 1.7 bilioni za Marekani nchini Tanzania hivyo basi kuunda nafasi 55,000 za ajira kwa Watanzania. Kwa mfano, benki tano za Kenya (KCB, Equity, Diamond Trust, I & M Holdings na NCBA Group) zimefungua matawi nchini Tanzania; na

j) Tangu Samia Suluhu Hassan awe rais, uhusiano wa kibashara na Tanzania umeboreka huku vikwazo visivyo vya ushuru vikitatuliwa.

45. Kenya na Tanzania zilifanya kikao chao cha nane cha pamoja cha Kamati ya Kiufundi ya Biashara jijini Kisumu, Kenya, mnamo Machi 2024. Lengo la kikao lilikuwa kuimarisha biashara kwa kuondoa vikwazo vyote visivyo vya ushuru. Matokeo mazuri ya kikao yaliidhinisha mikakati na makataa ya kuondoa vikwazo visivyo vya ushuru kufikia mwisho wa Juni 2024.

#### 4.2.5 Miradi na Mipango muhimu ya pamoja

46. Balozi aliangazia miradi na mipango muhimu ya pamoja inayoendelea kati ya Kenya na Tanzania. Miradi hii ni kama ifuatavyo: —

a) Bomba la kilomita 600 la gesi asili kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa;

b) Mradi wa Ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki unaofadhiliwa na African Development Bank (AfDB) unaounganisha Kenya na Tanzania (Barabara ya Malindi- Bagamoyo ya kilomita 454);

c) Mradi wa Usambazaji Umeme wa East Africa Power Pool (400KV Singida-Arusha- Namanga)

d) Kuthibitisha na kuweka mipaka ya kimaitafa.

### 4.3 Masuala ya Kigeni na Kibalozi

47. Ubalozi wa Kenya unatoa huduma za kibalozi kwa Wakenya wanaoishi Tanzania na raia wa kigeni wanaotaka kuzuru Kenya. Huduma hizi zinajumuisha: utoaji viza, stakabadhi za usafiri, vyeti vya madili mema kwa ushirikiano na DCI, kuthibitisha stakabadhi, kutoa vyeti vya kutangua, kutembelea wafungwa Wakenya na wagonjwa Wakenya hospitalini, kujibu maswali kutoka kwa Wakenya kwa mfano wahitaji, na mengineyo.

48. Ubalozi unaweka hifadhi ya Wakenya walio Tanzania na ina huduma ya mtandao ya usajili. Wakenya wanaosafiri au kuishi Tanzania wanaweza kujisajisali kwa kutumia kiungo kilicho katika wavuti ya Ubalozi. Kutokana na ukubwa wa Tanzania, mtandao huo umewawezesha Wakenya wanaoishi Tanzania kujisali bila ya kuja Ubalozini, hivyo basi kuwapunguzia muda na gharama za usafiri.
49. Ubalozi unafuatilia kuboresha kiungo cha takwimu kwenye mtandao huo wa usajili ukishirikiana na mitandao ya simu ili kupata kwa usahihi idadi ya Wakenya waliosalia Tanzania kwa muda mrefu na wale ambao wamerudi Kenya.
50. Kwa ushirikiano na benki ya KCB, Kenya Airways, Vodacom na washikadau wengine, Ubalozi uliandaa mkutano wa Wakenya walio Tanzania tarehe 9 Machi 2024 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulikuwa na kauli mbiu, "Kuukuza Mahusiano na Kuimarisha Uwezo wa Wakenya Waoishi Tanzania". Wakenya wanaoishi Tanzania walihamasishwa kuhusu mifumo na miundo iliyowekwa na serikali ya Kenya kuwalinda na kutumia fursa zilizoko, sera ya ughaibuni ya Kenya, huduma za ubalozi zinazotelewa na Ubalozi na fursa za uwekezaji nchini Kenya. Mkutano huo, ambao ulileta pamoja zaidi ya Wakenya 500 wanaoishi Tanzania, pia ulileta fursa muhimu za ajira, biashara na ubadilishanaji wa ujuzi na teknolojia.
51. Ubalozi uliandaa huduma tamba za ubalozi kati ya 26 na 27 Machi 2024. Idara ya Masuala ya Ughaibuni ikishirikiana na Idara ya Uhamiaji na Huduma za Umma zilipanga mkutano huo. Shughuli hiyo ilivutia Wakenya wengi ambao walisaidika kutuma maombi ya kupata paspoti mpya, vitambulisho, vyeti vya kuzaliwa na stakabadhi za usafiri wa dharura, na huduma za ubalozi na kadhalika.
52. Kwa muda mrefu sasa, imedhihirika kuwa raia walio ugenini huchangia pakubwa ustawi wa kiuchumi kwa kuwa wao ni chanzo cha fedha za kigeni. Fedha za kigeni zinazoingia Kenya zimekuwa zikiongezeka, kiwango hicho kikiwa asilimia 3 ya jumla ya pato la nchi (GDP). Ni muhimu kutambua kwamba barani Afrika, Tanzania inaongoza kuingiza fedha za kigeni nchini Kenya.

### 4.4 Fursa kwa Kenya

#### 4.4.1 Mradi wa gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa

53. Kufuatia kupatikana kwa kiwango kikubwa cha gesi asilia nchini Tanzania na kuwepo soko lake nchini Tanzania na Kenya, na kuzingatia mahitaji ya soko la Kenya ya gesi asilia, mnamo tarehe 4 Mei 2021, serikali za Tanzania na Kenya zilifikia mapatano ya kushirikiana katika kustawisha mradi huo wa gesi kutoka Tanzania kuja Kenya.
54. Rais wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Kenya Mhe. William Ruto walikubaliana kuharakisha ujenzi wa bomba la gesi asilia la kilomita 600 baina ya nchi hizo mbili. Mradi huo wa bomba unatarajiwa kuinua biashara baina ya mataifa hayo mawili ya Afrika na kupunguza gharama za kawi. Mradi huo unakisiwa kugharimu Ksh132 bilioni (Dola 1.1 bilioni za Marekani) na unatarajiwa kufadhiliwa kupitia ushurikiano wa serikali na mashirika ya binafsi (PPP). Mradi huo utawezesha Kenya kutumia hifadhi ya gesi asilia ya Tanzania hivyo kupunguza bei ya umeme na gesi ya kupikia.
55. Matayarisho ya utafiti wa uwezekano wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Mombasa yameanza. Kamati ya Kiufundi ya Pamoja (JTC) imeshakutana na wataalamu kutoka Kenya na Tanzania. Mkutano wa majuzi ulifanywa Februari 2023 jijini Dar es Salaam. Katika mkutano wa tatu wa JTC, stakabadhi kadhaa ziliandikwa na

kutamatishwa. Serikali za Kenya na Tanzania zishaafikiana na kutoa ruhusa. Kenya inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa nne wa JTC kwa robo ya kwanza ya 2024.

56. Kutiwa sahihi kwa rasimu ya makubaliano kati ya Kenya na Tanzania kuhusu utafiti wa uwezekano wa ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Dar es Salaam hadi Kenya kunatarajiwa kufanywa na Mawaziri wa Kawi wa nchi zote mbili mapema 2024 katika mkutano wa nne wa JTC.

#### 4.4.2 Kukuza Biashara na Uwekezaji wa Pamoja

57. Kuhusu hili, Balozi alisema hivi —

    a) Vikwazo visivyo vya ushuru vya mara kwa mara vimekuwa na athari ya kupunguza upitishaji huru wa bidhaa na watu kati ya Kenya na Tanzania. Hili likizingatiwa, Machi 2024, Kenya na Tanzania walifanya mkutano wa nane wa JTC kuhusu biashara jijini Kisumu, Kenya lengo likiwa ni kuimarisha biashara ya pamoja kwa kufutilia mbali vikwazo visivyo vya ushuru. Matokeo ya mkutano huo wa pamoja yalifana na kutoa mikakati na makataa ya kufutilia mbali vikwazo visivyo vya ushuru ifikapo mwisho wa Juni 2024.

    b) Ubalozi utaratibu, kuwezesha na kushiriki maonyesho ya kibiashara yajayo, pamoja na Maonyesho ya Kibiashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) ya 48 yatakayoandaliwa Juni 2024. Maonyesho hayo yanatarajiwa kuongeza ufahamu wa soko la bidhaa za Kenya zilizoko Tanzania.

    c) Ubalozi utazidi kuratibu na kuwezesha kushiriki kwa Kenya katika majukwaa ya biashara, maonyesho na shughuli zinazonadi bidhaa za Kenya ng'ambo na kuongeza ufahamu wa soko la bidhaa za Kenya zilizoko Tanzania.

    d) Ili kuongeza ufahamu wa fursa za kibiashara zilizoko, Ubalozi utaendelea kutoa taarifa za soko kwa makao makuu ya wizara na mashirika mengine husika ili ziwafikie watengezaji bidhaa wa Kenya na wauzaji bidhaa nchi za nje.

    e) Ubalozi utaunganisha wauzaji wawezao kuuza bidhaa nchi za nje kwa masoko ya Tanzania ili kupanua biashara ya Kenya nchini Tanzania na kuongeza ufahamu wa bidhaa za Kenya nchini Tanzania; na,

    f) Ubalozi utafanya mkutano na jamii ya wafanyabiashara wa Kenya nchini Tanzania kwa lengo la kubadilishana habari kuhusu fursa ili kulinda maslahi ya kibiashara na ya uwekezaji ya Kenya.

#### 4.4.3 Kudumisha Uwepo wa Kidiplomasia wa Kenya wa Masoko Mapya na Ibuka

58. Ubalozi umekubaliwa na Ushelisheli, Visiwa vya Ngazija, Mauritius na Muungano wa IORA. Ili kuimarisha uhusiano wa Kenya katika masoko mapya na ibuka, Kenya na Ushelisheli zilitia sahihi mkataba wa mahusiano mnamo Juni 2014. Kikao cha JCC cha kwanza baina ya Kenya na Ushelisheli kinatarajiwa kufanyika Kenya tarehe zitakazoafikiwa kidiplomasia. Kikao cha kwanza cha JCC baina ya Kenya na Visiwa vya Ngazija kinatarajiwa kufanyika tarehe 3 hadi 5 Juni 2024.

59. Wizara ya Afya ya Ushelisheli imeonyesha nia ya kuteua wataalamu wa afya kutoka Kenya kufanya kazi na Shirika la Afya la Ushelisheli kwa kandarasi za muda mfupi na mrefu. Wizara ya Afya inashughulikia ombi hilo.

#### 4.4.4 Utekelezaji wa Itifaki ya Jumuiya kuhusu Habari, Mawasiliano na Teknolojia

60. Nchi zote wanachama zimeridhia na zinatekeleza Itifaki ya Jumuiya kuhusu Habari, Mawasiliano na Teknolojia. Hata hivyo, Tanzania ingali haijasawazisha ada za mawasiliano za kutanga na nchi nyingine wanachama. Kuna haja ya kuendelea kurai Tanzania kufanya hivyo kwani hii itapunguza gharama ya mawasiliano ya kutanga hivyo kuchangia kupunguka kwa gharama ya kufanya biashara katika eneo hili

### 4.5 Masuala ya Utawala katika Balozi

#### 4.5.1 Raslimali kazi

61. Ubalozi wa Kenya Dar es Salaam unaongozwa na Balozi. Maafisa saba wa kisiasa wanafanya majukumu ya kidiplomasia. Watatu ni kutoka kwa Wizara, Idara na Mashirika (MDAs) husika ya serikali ya Kenya na wanatekeleza majukumu yao ipasavyo. Watatu hawa ni Mshauri wa Masuala ya Ulinzi, Afisa wa Mahusiano ya Kigeni, na Afisa wa Uhamiaji. Isitoshe, Ubalozi una wafanyakazi kumi na wawili (12) walioajiriwa kama maafisa wenyeji kutoa huduma za kawaida.

#### 4.5.2 Fedha na makadirio

62. Takwimu zifuatazo zinaonyesha fedha zilizotengewa Ubalozi kwa miaka mitatu iliyopita. Ingawa mahitaji ya kifedha ya Ubalozi yanaongezeka, fedha inazotengewa zimesalia zile zile kwa miaka kadha, hivyo basi kuifanya ipate changamoto katika utekelezaji wa mipango yake..

63. Aidha, Ubalozi unakumbwa na changamoto ya kucheleweshwa kwa marejesho ya ushuru kwa thamani kutoka kwa nchi mwenyeji.

| | MWAKA | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| MAKADIRIO | MATUMIZI YA JUMLA | 213,885,891.00 | 213,885,891.00 | 269,368,657 |
| | A-I-A | 36,584,600.00 | 37,699,600.00 | 57,482,300.00 |
| | MATUMIZI KAMILI | 177,301,291.00 | 176,186,291.00 | 251,886,357.00 |

#### 4.5.3 Usimamizi wa utendakazi

64. Ubalozi uko katika mchakato wa kuunda mpango-mkakati kwa kipindi cha 2023/24 hadi 2027/28 ambao utaorodhesha mipango inayotarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

65. Kandarasi ya utendakazi ya 2023/24 inatekelezwa. Hadi sasa, Ubalozi umefanikiwa kwa kiwango cha asilimia 80 katika utekelezaji wa malengo yake.

#### 4.5.4 Mali za serikali

66. Serikali ya Kenya inamiliki mali kadhaa nchini Tanzania, zikiwemo—

    a) Jengo la ghorofa mbili lililokodishiwa Benki ya KCB Tanzania (Harambee Plaza) Ploti Nambari 18582;

    b) Afisi za Ubalozi (Kenya House) Ploti Nambari 1859;

c) Nyumba mbili za makazi (zilizo kwenye Ploti Nambari 34987);

d) Nyumba ya ghorofa moja ya FRO kwenye Ploti Nambari 689- eneo la Mikocheni, Barabara ya Mawezi.

e) Ploti ya ekari tano jijini Dodoma.

67. Balozi na wafanyakazi wengine wote wanaishi kwenye nyumba za kukodisha ambazo ni ghali mno jijini Dar es Salaam. Ubalozi unapendekeza serikali inunue au ijenge makao ya Balozi.

#### 4.5.5 Magari

68. Ubalozi unamiliki magari matano ambapo manne ni aina ya Prado na moja ni vani. Ubalozi pia unamiliki pikipiki moja. Mbili kati ya Prado hizo ni za mashirika.

69. Magari mawili ya Ubalozi, yaani Toyota Land Cruiser Prado VX-L na vani zina miaka minane na miaka saba mtawalia na zimehudumu kwa mwendo mrefu. Magari hayo huenda mwendo mrefu kati ya Dar es Salaam na miji mingine ikiwemo Dodoma, Arusha na kadhalika yanapowasafirisha wafanyazi kwa hafla rasmi ambazo hufanywa nje ya Dar es Salaam. Hii hufanya gharama za kuzirekebisha kuwa juu mno.

70. Kwa hivyo Ubalozi unaomba utengewe fedha za kutosha katika mwaka wa kifedha wa 2023/24 ili kununua gari jingine kama hilo.

### 4.8 Changamoto za Ubalozi

71. Ubalozi unakumbwa na changamoto kadha katika utekelezaji wa mipango yake, zikiwemo—

a) Uhaba wa fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake katika nchi yenye kasi;

b) Vikwazo vya mara kwa mara visivyo vya ushuru ambavyo vimezorotesha biashara na kupunguza usafiri huru wa watu na bidhaa baina ya nchi hizi mbili;

c) Utekelezaji wa pole pole wa mipango na shughuli kadhaa za pamoja;

d) Kuwepo kwa ubaguzi na kasumba kuhusu utamaduni: kutoaminiana kumefanya Wakenya na kampuni za Kenya kupata ugumu kufanya kazi na kujipenyeza katika masoko ya Tanzania;

e) Tanzania haijatelekeleza kikamilifu baadhi ya Itifaki za Jumuiya kama vile Itifaki ya Soko Moja la Jumuiya. Kenya, Uganda na Rwanda ziliondoa ada za kupata vibali vya kufanya kazi na kurahisisha mchakato na mahitaji kwa raia wa nchi hizo tatu kupata vibali vya kufanya kazi ili kuwezesha ubalidilishanaji wa wafanyakazi. Wakenya wangali wanatozwa ada za kupata vibali vya kufanya kazi nchini Tanzania ilhali Kenya haitozi raia wa Jumuiya vibali hivyo. Kuna haja ya Kenya kuendelea kuirai Tanzania kutowatoza Wakenya vibali hivyo;

f) Kenya na Tanzania zina mpaka mkubwa ambao watu huvuka kiholela. Biashara haramu na aina tofauti za uhalifu wa kimataifa hufanyika mara kwa mara kupitia vichochoro vinavyojulikana kama *panya routes*. Biashara hii na ukosefu wa usalama zinaiharibia nchi jina;

g) Ukuaji wa upesi wa teknolojia unahatarisha usalama wa data ya Ubalozi ambayo huhifadhiwa na hutumwa kielektroniki;

h) Athari za mabadiliko ya tabianchi duniani kote na majanga asilia kama vile mafuriko na ukame husababisha uharibifu wa miundomsingi, mali, na kufanya gharama ya maisha kupanda.

## 5.0 YALIYOGUNDULIWA

72. Ujumbe uligundua yafuatayo—

a) Kamati iligundua kwamba EAKC imefanya uchambuzi wa uhitaji wa mafunzo ya Kiswahili na imekusudia kuanza mafunzo ya Kiswahili ndani ya nchi zote wanachama ambazo zilitambua changamoto zinazokabili maendeleo na uenezaji Kiswahili katika Jumuiya;

b) Tume hii ya Kiswahili yafaa kuunga mkono hamasa na mbinu za kujijulisha kwa washikadau muhimu ambao ni pamoja na Bunge la Kenya;

c) Wakenya walio nchini Tanzania kulipa viza za biashara kila miezi mitatu si sawasawa na itifaki za upitishaji huru wa bidhaa na huduma. Yafaa suala hili litatuliwe kidiplomasia.

d) Tofauti ya malipo kwa huduma za uchukuzi katika bandari za Tanzania yafaa kuangaliwa. Wakenya hutakiwa kulipa Dola 35 za Marekani kwa tiketi ya kawaida kutoka Dar es Salaam hadi Zanzibar huku Watanzania wakilipa Tsh30,000 tu. Kamati ya Ufundi ya Uchukuzi yafaa kutatua hili ili kuwepo usawa katika kiwango kinacholipwa na kila mmoja;

e) Vibali vya biashara kwa Wakenya walio Tanzania na uwezo mahususi wa mtaji-hisa kusajili biashara vyafaa kurekebishwa ili kufutilia mbali vibali vya biashara na kushusha uhitaji wa kiwango cha mtaji-hisa kama ifanyavyo Kenya. Hii itawezesha wawekezaji wadogo kuwekeza nchini Tanzania, kusajili biashara zao pale, na kupata mikopo kutoka kwa asasi za kifedha. Yafaa Kamati ya Kiufundi ya Leba na Uhamiaji, pamoja na Kamati ya Kiufundi ya Biashara, kubainisha suala hili ili lijadiliwe.

f) Viza za biashara zitolewazo mipakani pekee hugharimu Dola 100 za Marekani na hulazimu Wakenya kusafiri hadi mipakani kila baada ya miezi mitatu ili kujiandikisha tena. Malipo haya yanafaa kufanywa nafuu au kufutiliwa mbali. Pia, kuwepo vituo vya kujiandikisha nchini Zanzibar ili kuepuka gharama ya kulazimika kusafiri hadi mipakani kila baada ya miezi mitatu. Isitoshe, viza hazifai kuisha kila mtu atokapo Tanzania hata kabla ya miezi mitatu kama ilivyo.

g) Mgao wa fedha kwa balozi na juhudi nyingine za nje ya nchi wafaa kulingana na kazi na mipango ya balozi au juhudi mahususi. Uzito wa biashara na masuala katika kila balozi wafaa kuamua kiasi cha mgao.

h) Kenya na Tanzania zimeendelea kuimarisha uhusiano wao. Hivyo, ipo haja kukoleza mazungumzo ya kidiplomasia baina ya nchi hizi ili kuboresha sheria zao kuhimiza uwekezaji zaidi.

i) Umma wa nchi wanachama hauna ufahamu wa kutosha kuhusu matendo na mipango ya EAKC kustawisha dhima ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya mawasiliano katika Jumuiya.

## 6.0 MATOKEO NA MAPENDEKEZO

73. Katika muktadha wa Jumuiya, Kamati inapendekeza yafuatayo—

a) **Mgao wa Fedha kwa Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (EAKC)** – Kamati inapendekeza kwamba Tume ya Kiswahili ya Afrika Mashariki, kama kitengo cha Jumuiya, yafaa ipewe fedha na wafanyakazi wa kutosha ili itekeleze wajibu wake kwa ufanisi. Isitoshe, Kamati inashauri Wizara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sehemu Kame na Ustawi wa Kikanda ishirikiane na Wizara ya Masuala ya Kigeni na Ughaibuni kuhakikisha vitengo na asasi zote za Jumuiya zipewe fedha na wafanyakazi wa kutosha. Haswa EAKC.

b) **EAKC Kutoa Mafunzo na Kuwezesha Bunge** - Uongozi wa Bunge wafaa kuunga mkono lengo la EAKC la kutoa mafunzo ya Kiswahili kwa Wabunge na wafanyakazi kuhusu matumizi ya Kiswahili bungeni.

c) **Upitishaji Huru wa Bidhaa na Huduma**- Kamati inapendekeza Wakenya walio nchini Tanzania kuajiriwa na kufanya biashara bila vikwazo vya vibali, idhini, nk. Hili litaimarisha nguvukazi ya Jumuiya na kukuza mitaji. Wizara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sehemu Kame na Ustawi wa Kikanda ishirikiane na Wizara ya Masuala ya Kigeni na Ughaibuni zitumie diplomasia kutatua suala la kulipa vibali vya biashara kila miezi mitatu.

d) **Vikwazo kwa Biashara visivyo vya ushuru** – Jumuiya iunde mfumo wa kutatua vikwazo visivyo vya ushuru ifikapo Juni 2024 ili kuwezesha upitishaji huru wa watu, bidhaa, na huduma kati ya nchi hizi mbili;

e) **Viza za Biashara**– Kamati inapendekeza kurekebisha na kushusha bei ya viza za biashara au kuzifutilia mbali. Kuwepo Zanzibar, vituo vya kusajili viza hizo upya ili kuepuka gharama ya kusafiri hadi mipakani kusajili viza hizo kila miezi mitatu. Isitoshe, muda wa viza haufai kuisha kila mtu atokapo Tanzania kabla ya miezi mitatu kama ilivyo. Yafaa suala hili liwekwe wazi mbele ya Kamati ya Kiufundi ya Leba na Huduma za Uhamiaji, pia mbele ya Kamati ya Kiufundi ya Kaida za Biashara, lijadiliwe ili kupata suluhisho kabla ya Mwaka wa Kifedha wa 2024/2025 kukamilika;

f) **Fedha kwa Balozi** – Fedha kwa kila Balozi zafaa kulingana na kazi na mipango yake. Kiasi cha biashara na ukubwa wa masuala katika kila balozi uamue kiasi cha mgao. Ili balozi zitumike ifaavyo, Wizara ya Masuala ya Kigeni na Ughaibuni yafaa kuongeza mgao wakati wa mijadala kuhusu Makadirio ya Mwaka wa Kifedha wa 2024/2025.

g) **Masuala Ibuka** - Kamati inashauri nchi wanachama kuchangamkia masuala yanayoibuka katika eneo la Jumuiya. Zikizingatia mabadiliko ya hali ya kila mara na fursa zinazoibuka, nchi wanachama zafaa kuwa macho ili kunufaisha nchi mbili na nyinginezo.

h) **Ubalozi uhamie Dodoma** - Serikali ya Tanzania imetenga ardhi ya kujenga Ubalozi wa Kenya mjini Dodoma. Kamati inapendekeza ujenzi huo uharakishwe ili kupunguza gharama ya shughuli. Waziri atenge fedha katika Mwaka wa Kifedha wa 2024/2025.

i) **Kuimarisha Mahusiano ya Pamoja** - Kamati inapendekeza kwamba Kenya na Tanzania ziendelee kuimarisha uhusiano wao kwa kusisitiza mipango ya mara kwa mara ya ubadilishanaji, juhudi za ushirikiano, na mazungumzo ya ngazi za juu.

**Sahihi:** ......[signature]...... **Tarehe:** 1ST APRIL, 2025

**MHE. CS IRENE MAYAKA, MBUNGE – MWENYEKITI**

**VIAMBATISHO**

1. Orodha ya kuidhinisha
2. Kumbukumbu

THE NATIONAL ASSEMBLY
PAPERS LAID
DATE: 09 APR 2025
TABLED BY:

**KAMATI YA UTANGAMANO WA KIKANDA**

**Orodha ya Uidhinishaji**

Uidhinishaji wa Ripoti ya Ziara ya Ukaguzi wa Asasi Zisizojitegemea Kikamilifu za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ukanda wa Kati katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Sisi ambao majina yetu yameambatishwa kwenye Ripoti hii, sasa tunatia sahihi zetu Ripoti hii kuthibitisha kwamba tunaiidhinisha.

| NMB. | MHESHIMIWA | SAHIHI |
|---|---|---|
| 1. | Hon. CS Mayaka Irene Nyakerario, MP- **Chairperson** | [signature] |
| 2. | Hon. Farah Salah, MP – **Vice Chairperson** | [signature] |
| 3. | Hon. David Ochieng', CBS, MP | |
| 4. | Hon. Naomi Waqo, CBS, MP | [signature] |
| 5. | Hon. (Dr.) Makali Mulu, CBS, MP | [signature] |
| 6. | Hon. Wanjiku Muhia, CBS, MP | [signature] |
| 7. | Hon. Geoffrey Makokha Odanga, MP | |
| 8. | Hon. Joseph Gitari, MP | [signature] |
| 9. | Hon. Danson Mwashako, MP | [signature] |
| 10. | Hon. Andrew Adipo Okuome, MP | [signature] |
| 11. | Hon. Christopher Aseka Wangaya, MP | [signature] |
| 12. | Hon. Rael Chepkemoi Kasiwai, MP | [signature] |
| 13. | Hon. Elizabeth Karambu Kailemia, MP | [signature] |
| 14. | Hon. Beatrice Chepng'eno Kemei, MP | |
| 15. | Hon. Fatuma Hamisi Masito, MP | |
| 16. | Hon. Irene Njoki Mrembo, MP | |
| 17. | Hon. CPA Julius Kipletting Rutto, MP | |
| 18. | Hon. Richard Kipkemoi Yegon, MP | [signature] |
| 19. | Hon. Japheth Nyakundi Mokaya, MP | |
| 20. | Hon. Zaheer Jhanda, MP | |
| 21. | Hon. Didmus Barasa Mutua, MP | |